JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MWONGOZO WA ELIMU YA MPIGA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2024

**Umeandaliwa na:**
Ofisi ya Rais, TAMISEMI,
Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S. L. P 1923,
41185 DODOMA.
Simu: (26) 2322607
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz

# DIBAJI



Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Madhumuni ya kuwepo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni utekelezaji wa dhana ya ugatuaji wa madaraka, ambayo inalenga kupeleka madaraka ya kisiasa kwa wananchi. Hivyo, pamoja na shughuli nyingine, Serikali za Mitaa zina wajibu wa kuimarisha demokrasia katika maeneo yao na kuitumia demokrasia hiyo kuharakisha maendeleo ya wananchi. Kwa mantiki hiyo, msingi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hufanyika kila baada ya miaka mitano kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288. Uchaguzi utakaofanyika mwaka 2024 utakuwa wa saba tangu kurejeshwa kwa mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa nchini Tanzania mwaka 1992. Katika Uchaguzi huo, wananchi watapata fursa ya kuchagua Wenyeviti wa Vijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Wajumbe wa Kamati za Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji. Hivyo, kufanyika kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kunawezesha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba ya kuomba kuongoza wenzao na kuchagua viongozi wa maeneo wanayoishi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina jukumu la kusimamia na kuratibu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Ofisi ya Rais, TAMISEMI hutekeleza jukumu hilo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Uchaguzi ili kuongeza uwazi, ufanisi na uwajibikaji. Katika kutekeleza jukumu hilo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeandaa Miongozo mbalimbali ukiwemo Mwongozo huu wa Elimu ya Mpiga Kura utakaotumiwa na wadau wote wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa wananchi. Lengo la Elimu ya Mpiga Kura ni kuwawezesha na kuwahamasisha wananchi na wadau wa Uchaguzi kuelewa mchakato wote wa Uchaguzi, kanuni na taratibu muhimu za Serikali za Mitaa ili waweze kushiriki na kutumia vyema haki yao ya Kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa katika nafasi za uongozi wa Serikali za Mitaa katika maeneo yote Tanzania Bara.

**Mohamed Omari Mchengerwa (Mb),**
**Waziri wa Nchi,**
**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
**Agosti, 2024**

**YALIYOMO**


DIBAJI ..... i

SURA YA KWANZA ..... 1

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Muundo wa Mwongozo ..... 1

1.3 Serikali za Mitaa ..... 1

1.4 Muundo wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara ..... 2

1.5 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ..... 2

1.6 Sheria na Kanuni Zinazosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ..... 5

1.7 Mfumo wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ..... 5

1.8 Vipindi au Mzunguko wa Uchaguzi ..... 5

SURA YA PILI ..... 7

TANGAZO LA UCHAGUZI NA ORODHA YA MAENEO YA UCHAGUZI ..... 7

**2.1 Utangulizi** ..... 7

**2.2 Mamlaka na Taratibu za Kutoa Tangazo la Uchaguzi** ..... 7

**2.3 Majina na Mipaka ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa** ..... 8

**2.4 Nafasi zinazogombewa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa** ..... 8

SURA YA TATU ..... 10

ELIMU YA MPIGA KURA ..... 10

3.1 Utangulizi. ..... 10

3.2 Maana ya Elimu ya Mpiga Kura ..... 10

3.3 Malengo ya Elimu ya Mpiga Kura ..... 10

3.4 Mamlaka ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Katika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura . 11

3.5 Vigezo Vinavyotumika Katika Kutoa Vibali ..... 11

3.6 Nyaraka Muhimu za Kuambatisha Kwenye Maombi ya Kibali ..... 12

3.7 Wadau wa Elimu ya Mpiga Kura. ..... 12

3.8 Wajibu wa Wadau ..... 13

3.9 Mambo Yasiyoruhusiwa Kufanywa na Wadau wa Elimu ya Mpiga Kura .... 14
3.10 Njia Zinazotumika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura .... 14
3.11 Makundi Maalum .... 15
SURA YA NNE .... 21
UANDIKISHAJI NA UANDAAJI WA ORODHA YA WAPIGA KURA .... 21
4.1 Utangulizi .... 21
4.2 Sifa za Kuandikishwa katika Orodha ya Mpiga Kura .... 22
4.3 Mahali na muda wa uandikishaji wapiga kura .... 22
4.4 Uhakiki wa orodha ya wapiga kura .... 22
4.5 Uteuzi wa waandikishaji na waandaaji wa orodha ya wapiga kura .... 23
4.6 Mawakala wa uandikishaji wa Wapiga Kura .... 23
4.7 Pingamizi kuhusu Uandikishaji .... 23
4.8 Fomu zinazotumika katika uchaguzi .... 24
SURA YA TANO .... 25
UTEUZI, PINGAMIZI NA RUFAA ZA WAGOMBEA .... 25
5.1 Utangulizi .... 25
5.2 Sifa za Mgombea .... 25
5.3 Kukosa Sifa ya Kuwa Mgombea .... 25
5.4 Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi .... 26
5.5 Utaratibu wa Uteuzi wa Wagombea .... 26
5.6 Utaratibu wa Uteuzi wa Mgombea Pekee .... 27
5.7 Pingamizi Dhidi ya Wagombea .... 27
5.8 Taratibu za Kushughulikia Rufaa .... 27
5.9 Kifo kwa Mgombea .... 28
5.10 Kujitoa kwa Mgombea .... 28
5.11 Fomu za Maombi ya Uteuzi .... 28
SURA YA SITA .... 29
KAMPENI ZA UCHAGUZI .... 29
6.1 Utangulizi .... 29

6.2 Mambo muhimu ya kuzingatia ........ 29
6.3 Wajibu wa Wadau wa Uchaguzi wakati wa Kampeni ........ 30
6.4 Taratibu za Maadili ........ 31
6.5 Kamati za Maadili ya Uchaguzi ........ 33
6.6 Rufaa Dhidi ya Maamuzi ........ 34
6.7 Malalamiko dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ........ 34
6.8 Uwasilishwaji wa Malalamiko ya Ukiukwaji wa Maadili ........ 34
SURA YA SABA ........ 36
TARATIBU ZA UPIGAJI KURA ........ 36
7.1 Utangulizi ........ 36
7.2 Sifa za Mpiga Kura ........ 36
7.3 Mahali, Vituo na Muda wa Kupiga Kura ........ 36
7.4 Masanduku ya Kura ........ 37
7.5 Karatasi za Kupigia Kura ........ 37
7.6 Utambulisho wa Mpiga Kura ........ 37
7.7 Upigaji Kura ........ 38
7.8 Usaidizi kwa Wenye Mahitaji Maalum ........ 38
7.9 Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Kupiga Kura ........ 38
7.10 Watu Wanaoruhusiwa Kuingia Kwenye Kituo cha Kupiga Kura ........ 39
SURA YA NANE ........ 40
KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO ........ 40
8.1 Utangulizi ........ 40
8.2 Wanaopaswa Kuwepo Wakati wa Kuhesabu Kura na Kujumlisha Matokeo 40
8.3 Kuhesabu Kura ........ 40
8.4 Kura Zitakazohesabiwa Kuwa Zimekataliwa ........ 41
8.5 Kujumlisha na Kutangaza Matokeo ........ 41
SURA YA TISA ........ 43
MAWAKALA NA WAANGALIZI WA UCHAGUZI ........ 43

9.1 Utangulizi ........ 43
9.2 Wakala wa Vyama vya Siasa Kwenye Uchaguzi ........ 43
9.3 Vigezo vya kuwa Wakala wa Chama cha Siasa: ........ 43
9.4 Jukumu la Wakala wa Chama cha Siasa: ........ 44
9.5 Waangalizi wa Uchaguzi ........ 44
9.6 Vigezo vya kuwa Mwangalizi wa Ndani wa Uchaguzi ........ 44
9.7 Wajibu wa Waangalizi ........ 44
SURA YA KUMI ........ 46
MAKOSA NA ADHABU ........ 46
10.1 Utangulizi ........ 46
10.2 Makosa ya Uchaguzi ........ 46
10.3 Adhabu: ........ 47
10.4 Adhabu kwa kukiuka Taratibu za Maadili ya Uchaguzi ........ 47

# SURA YA KWANZA

## OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

### 1.1 Utangulizi

Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura umelenga kuelimisha, kuwezesha na kuhamasisha wapiga kura na wadau watakaopewa jukumu la kutoa Elimu ya Mpiga Kura kuhusu mchakato wa uchaguzi, kanuni, haki na wajibu wao katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Mwaka 2024. Aidha, Mwongozo umefafanua majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na wadau wengine katika kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

### 1.2 Muundo wa Mwongozo

Mwongozo huu umegawanyika katika Sura Kumi ambazo ni: utangulizi, tangazo la uchaguzi na orodha ya maeneo ya uchaguzi, elimu ya mpiga kura, uandikishaji na uandaaji wa orodha ya wapiga kura, uteuzi, pingamizi na rufaa za wagombea, kampeni za uchaguzi, taratibu za upigaji kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo, mawakala na waangalizi wa uchaguzi na makosa na adhabu.

### 1.3 Serikali za Mitaa

Serikali za Mitaa zimeanzishwa kwa mujibu wa Ibara 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inaeleza kuwa, vitaanzishwa vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila mkoa, wilaya, mji na kijiji, katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambavyo vitakuwa vya aina na majina yatakayowekwa na Sheria iliyotungwa na Bunge. Aidha, Ibara ndogo ya (2) inaeleza kuwa; Bunge au Baraza la Wawakilishi, kadri itakavyokuwa, litatunga Sheria itakayofafanua utaratibu wa kuanzisha vyombo vya Serikali za Mitaa; miundo na wajumbe wake, njia za mapato na utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za vyombo hivyo.

Vilevile, Ibara ya 146 (2) (a)–(c), inaeleza kuwa, madhumuni ya kuwapo Serikali ya Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi. Na kwamba, vyombo vya Serikali za Mitaa

vitakuwa na haki na mamlaka ya kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao. Hivyo, majukumu ya Serikali za Mitaa ni kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa katika eneo lake, kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na ulinzi wa wananchi, kuimarisha demokrasi katika eneo lake na kuitumia demokrasia ili kuharakisha maendeleo ya wananchi.

### 1.4 Muundo wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara

Muundo wa Serikali za Mitaa, Tanzania Bara unajumuisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tawala za Mikoa inajumuisha Mikoa, Wilaya na Tarafa. Serikali za Mitaa inajumuisha Mamlaka za Miji na Mamlaka za Wilaya. Aidha, Mamlaka za Miji zinahusisha Halmashauri za Majiji, Halmashauri za Manispaa na Halmashauri za Miji ambazo huundwa na Kata, Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Vilevile, Mamlaka za Wilaya zinahusisha Halmashauri za Wilaya zinazoundwa na Kata, Vijiji na Vitongoji. Pia, katika Halmashauri za Wilaya kuna Mamlaka za Miji Midogo ambazo zinaundwa na Kata na Vitongoji.

### 1.5 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Msingi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ambayo imeweka Serikali za Mitaa na kueleza kuwa madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa ni utekelezaji wa dhana ya ugatuaji wa madaraka yakiwepo ya kisiasa kwa wananchi. Hivyo, pamoja na shughuli nyingine, Serikali za Mitaa zina wajibu wa kuimarisha demokrasia katika maeneo yao na kuitumia demokrasia hiyo kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Kwa upande wa Tanzania Bara, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288 na kwa mujibu wa sheria hizi uchaguzi huo hufanyika kila baada ya miaka mitano. Uchaguzi utakaofanyika mwaka 2024 utakuwa wa saba tangu kurejeshwa kwa mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa nchini Tanzania mwaka 1992.

### 1.5.1 Majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Dira ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kuwa na Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zenye uwezo wa kutoa huduma bora kwa wananchi. Aidha, Dhima ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kuratibu, kuwezesha na kusimamia Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi kwa kutoa sera, miongozo na maelekezo ili kuwepo na huduma zilizoboreshwa.

Majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yameainishwa katika sheria mbalimbali. Kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288, Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa amepewa mamlaka ya kufanya yafuatayo:

i) Kusimamia na kuratibu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa;

ii) Kutengeneza Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kila Uchaguzi unapofanyika *kwa mujibu wa kifungu cha 201A cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya)* Sura 287*; na kifungu cha 87A cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji)* Sura 288;

iii) Kuandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura kwa mujibu wa *Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024*;

iv) Kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya mpiga kura;

v) Kuandaa na kutangaza orodha ya maeneo ya utawala yatakayohusika katika Uchaguzi kwa mujibu wa *Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024*; na

vi) Kutoa Tangazo la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

### 1.5.2 Jukumu la Tawala za Mikoa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa Sura 97 jukumu la Tawala za Mikoa ni kusimamia na kushauri Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuhakikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unafanyika katika hali ya utulivu na amani ili kupata ufanisi unaotakiwa.

### 1.5.3 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yameainishwa katika Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo (Tangazo la Serikali Na. 572 la Mwaka 2024); Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya, (Tangazo la Serikali Na. 571 la Mwaka 2024); Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji, (Tangazo la Serikali Na. 573 la Mwaka 2024); na Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji (Tangazo la Serikali Na. 574 la Mwaka 2024). Kwa mujibu wa kanuni hizi majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

i) Kutoa maelekezo ya uchaguzi siku sitini na mbili kabla ya siku ya uchaguzi kwa mujibu wa kanuni;
ii) Kutoa elimu ya mpiga kura pamoja na kuratibu na kusimamia wadau wanaotoa elimu ya mpiga kura ndani ya eneo la halmashauri;
iii) Kuandaa orodha ya wapiga kura kwa mujibu wa kanuni;
iv) Kuratibu mchakato wa uteuzi wa wagombea;
v) Kuratibu na kusimamia ratiba za kampeni za wagombea;
vi) Kushughulikia malalamiko na migogoro inayoweza kujitokeza wakati na baada ya uchaguzi;
vii) Kuandaa vituo na vifaa vya kupigia kura;

viii) Kuhesabu kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi katika eneo husika; na

ix) Kutunza vifaa na nyaraka za uchaguzi.

### 1.6 Sheria na Kanuni Zinazosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unasimamiwa na Sheria na Kanuni zifuatazo:

i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

ii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287;

iii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288;

iv) Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo (Tangazo la Serikali Na. 572la Mwaka 2024);

v) Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya, (Tangazo la Serikali Na. 571 la Mwaka 2024);

vi) Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji, (Tangazo la Serikali Na. 573 la Mwaka 2024); na

vii) Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji (Tangazo la Serikali Na. 574 la Mwaka 2024);

### 1.7 Mfumo wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024, Mgombea wa nafasi yoyote katika Serikali za Mitaa atatangazwa kuwa mshindi endapo atapata kura nyingi kuliko mgombea au wagombea wengine *(First-Past –the Post)*. Aidha, iwapo kuna mgombea pekee atatangazwa kuwa mshindi endapo atapata kura nyingi za ndio kuliko kura za hapana.

### 1.8 Vipindi au Mzunguko wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa kifungu 57 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na kifungu 16 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288 Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Mitaa unapaswa kufanyika kila baada ya miaka mitano.

**Maswali**

1. Serikali za Mitaa ni nini?
2. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hufanyika kila baada ya miaka mingapi?
3. Taasisi ipi ina mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa?
4. Taja majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.
5. Nani mwenye jukumu la kutangaza kwa umma juu ya uwepo wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa?
6. Taja majukumu ya Tawala za Mikoa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.
7. Taja majukumu ya Serikali za Mitaa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.
8. Nani mwenye mamlaka ya kuandaa Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura?
9. Zitaje sheria na kanuni zinazosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

# SURA YA PILI

# TANGAZO LA UCHAGUZI NA ORODHA YA MAENEO YA UCHAGUZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua kuhusu mamlaka na taratibu za kutoa tangazo la uchaguzi, majina na mipaka ya vijiji, mitaa na vitongoji na nafasi zitakazogombewa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Aidha, maudhui, yanalenga kuelimisha wananchi kuhusu: mamlaka na taratibu za kutoa tangazo la uchaguzi; muda wa kutolewa tangazo la uchaguzi; umuhimu wa kufahamu majina na mipaka ya maeneo ya uchaguzi; na kufahamu nafasi zinazogombewa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Lengo ni kwa wananchi wenye sifa kujitokeza na kutumia haki yao ya kikatiba na kisheria ya kuchagua na kuchaguliwa.

## 2.2 Mamlaka na Taratibu za Kutoa Tangazo la Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024, Waziri mwenye dhamana na Mamlaka za Serikali za Mitaa atatoa Tangazo la Uchaguzi kwa umma si chini ya siku 90 kabla ya siku ya uchaguzi ili kuwafahamisha wananchi kuhusu Uchaguzi wa wenyekiti wa vijiji, wajumbe wa halmashauri za vijiji, wajumbe wa halmashauri za vijiji kundi maalum la wanawake, wenyeviti wa vitongoji katika vijiji, wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za miji midogo, wenyeviti wa mitaa na wajumbe wa kamati za mitaa. Tangazo hilo litatolewa katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchi nzima na katika vyombo vingine vya habari. Tangazo litakalotolewa litaelekeza mambo muhimu yafuatayo:

i) Ratiba ya Uchaguzi na shughuli zinazohusika na uchaguzi; na

ii) Masharti muhimu ya uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za uchaguzi.

### 2.3 Majina na Mipaka ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024, Msimamizi wa Uchaguzi atabandika matangazo ya majina na mipaka ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa katika eneo lake katika sehemu ya wazi si chini ya siku 72 kabla ya uchaguzi.

### 2.4 Nafasi zinazogombewa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Nafasi zinazogombewa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hutegemea aina ya Halmashauri inayofanya uchaguzi kama ni Mamlaka ya Wilaya au Mji.

#### 2.4.1 Uchaguzi katika Mamlaka za Wilaya

Nafasi za uongozi zinazogombewa katika Mamlaka za Wilaya kwenye ngazi ya kijiji ni kama ifuatavyo:

i) Mwenyekiti wa Kijiji;
ii) Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake;
iii) Wajumbe 8 wa Halmashauri ya Kijiji kundi la wanawake ambao idadi yao itakuwa si chini ya theluthi moja ya wajumbe wote waliochaguliwa; na
iv) Wenyeviti wa Vitongoji.

Idadi ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji haitazidi wajumbe ishirini na tano.

#### 2.4.2 Uchaguzi katika Mamlaka za Miji Midogo

Nafasi ya uongozi inayogombewa katika mamlaka za miji midogo ni mwenyekiti wa kitongoji. Nafasi nyingine kama vile mwenyekiti wa mamlaka ya mji mdogo kwa mujibu wa Kifungu cha 45(1)(a) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, huchaguliwa na wajumbe wa Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo kutoka miongoni mwa wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka ya mji mdogo.

Nafasi ya wajumbe wanawake ambao ni robo ya wajumbe wa baraza la mamlaka ya mji mdogo kwa mujibu wa kifungu cha 45(1)(e) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 hupatikana kwa kupendekezwa na vyama vya siasa kwa kuzingatia idadi ya nafasi za wenyeviti wa vitongoji zilizochukuliwa na chama cha siasa. Hivyo, ni muhimu kuzingatia kuwa nafasi inayogombewa katika mamlaka ya mji mdogo ni moja tu, na ni nafasi ya mwenyekiti wa kitongoji.

### 2.4.3 Uchaguzi katika Mamlaka za Miji

Nafasi za uongozi zitakazogombewa katika ngazi ya mtaa ni zifuatazo:

i) Mwenyekiti wa Mtaa; na
ii) Wajumbe watano wa Kamati ya Mtaa ambao kati yao wawili watakuwa wanawake.

### 2.4.4 Uchaguzi kwenye Vijiji Vilivyopo katika Mamlaka za Miji

Nafasi za uongozi zitakazogombewa katika ngazi ya kijiji ni kama ifuatavyo:

i) Mwenyekiti wa Kijiji;
ii) Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake;
iii) Wajumbe 8 wa Halmashauri ya Kijiji kundi la wanawake ambao idadi yao inapaswa kuwa si chini ya theluthi moja ya wajumbe wote waliochaguliwa; na
iv) Wenyeviti wa Vitongoji.

Idadi ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji haitazidi wajumbe ishirini na tano.

**Maswali:**

1. Tangazo la uchaguzi wa Serikali za Mitaa linatolewa na nani na lini?
2. Ni nani anatoa tangazo la majina na mipaka ya vijiji, vitongoji na mitaa katika maeneo ya uchaguzi?
3. Je! Unafahamu maeneo yanayohusika na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa?
4. Taja nafasi zinazogombewa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa?
5. Taja idadi ya wajumbe wanaohitajika katika kundi la wanawake katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika mamlaka za wilaya na mamlaka za miji?
6. Je, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo hupatikanaje?

## SURA YA TATU

## ELIMU YA MPIGA KURA

### 3.1 Utangulizi.

Sura hii inaelezea maana ya Elimu ya Mpiga Kura; malengo ya Elimu ya Mpiga Kura; na umuhimu wa Elimu ya Mpiga Kura. Aidha, inafafanua utaratibu wa kuratibu utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura; njia zinazotumika kutoa Elimu ya Mpiga Kura; sifa zinazohitajika na vigezo vya kupata kibali cha kutoa Elimu ya Mpiga Kura. Vilevile sura hii inatoa ufafanuzi wa wadau wa Elimu ya Mpiga Kura; wajibu wa mdau anayetoa elimu kwa mpiga kura; na miiko katika kutoa elimu hiyo. Hivyo, katika Sura hii wananchi na wadau watakuwa na uelewa kuhusu: maana, malengo na umuhimu wa Elimu ya Mpiga Kura; uratibu wa Elimu ya Mpiga Kura; ushiriki wa wadau wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura; na mambo muhimu ya kuzingatia katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

### 3.2 Maana ya Elimu ya Mpiga Kura

Elimu ya Mpiga Kura ni elimu ambayo hutolewa kwa wananchi kwa lengo la kuwawezesha kuelewa taratibu za Uchaguzi, wajibu wao na umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi.

### 3.3 Malengo ya Elimu ya Mpiga Kura

Elimu ya mpiga kura inalenga:

i) Kuwasaidia wapiga kura na wadau wengine wa Uchaguzi kuzielewa vema Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayotumika kusimamia Uchaguzi;

ii) Kuwawezesha wananchi na wadau wengine kuelewa taratibu za Uchaguzi na kutumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa; na

iii) Kuwawezesha wananchi na wadau wengine wa Uchaguzi kupata taarifa sahihi kuhusu Uchaguzi.

### 3.4 Mamlaka ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatoa na kusimamia utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kwa mamlaka iliyopewa na Kanuni zifutazo:

i) Kanuni ya 54 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2024;

ii) Kanuni ya 54 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji Katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2024;

iii) Kanuni ya 51 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji Katika Mamlaka za Miji Midogo za Mwaka 2024; na

iv) Kanuni ya 53 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa Katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2024.

Katika kusimamia utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura, Ofisi ya Rais TAMISEMI ina wajibu wa:

i) Kuandaa Mwongozo wa kutoa Elimu ya Mpiga Kura na kuusambaza kwa wadau husika;
ii) Kupokea maombi na kutoa kibali kwa mdau anayetaka kutoa Elimu ya Mpiga Kura, ikiwa amekidhi vigezo;
iii) Kusimamia utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura ili kuhakikisha elimu hiyo inatolewa kwa usahihi na inawafikia walengwa waliokusudiwa; na
iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura.

### 3.5 Vigezo Vinavyotumika Katika Kutoa Vibali

Taasisi inayotaka kutoa Elimu ya Mpiga Kura itapaswa kuomba kibali kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

i) Kuwa na usajili kwa mujibu wa Sheria za Nchi;

ii) Iwe imefanya kazi nchini si chini ya miezi sita (6) tangu kusajiliwa kwake;
iii) Miongoni mwa watendaji wake wakuu, angalau wawili wanapaswa wawe Watanzania;
iv) Iwe haijawahi kujihusisha na vitendo vya kuvuruga amani au kuchochea fujo;
v) Kuwa tayari kufanya kazi katika eneo lolote Tanzania Bara endapo eneo ililokusudia kutoa Elimu ya Mpiga Kura tayari litakuwa na wadau wa kutosha;
vi) Iwe tayari kufanyiwa ukaguzi wakati wowote; na
vii) Kuwa na uwezo wa Kutoa Elimu ya Mpiga kura kwa gharama zake.

### 3.6 Nyaraka Muhimu za Kuambatisha Kwenye Maombi ya Kibali

Maombi ya Kibali yataambatishwa na taarifa muhimu zifuatazo:

i) Cheti cha Usajili;
ii) Barua kutoka Mamlaka ya usajili kuthibitisha uhai wa taasisi hiyo;
iii) Katiba ya taasisi;
iv) Majina, wasifu na namba za simu za viongozi wa juu wa taasisi na uthibitisho wa uraia wao;
v) Anuani ya makazi na namba za simu za taasisi;
vi) Taarifa ya fedha ya miaka mitatu ikionesha vyanzo vya fedha;
vii) Taarifa ya rasimaliwatu na vitendea kazi;
viii) Taarifa ya utendaji kazi;
ix) Vibali vya kazi na ukaazi endapo taasisi ina wafanyakazi ambao siyo raia wa Tanzania;
x) Taarifa za wadau/washirika wa karibu; na
xi) Taarifa nyingine muhimu kadri zitakavyohitajika na Ofisi ya Rais, TAMISEMI

### 3.7 Wadau wa Elimu ya Mpiga Kura.

Katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itashirikiana na Wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata elimu hiyo. Wadau hao ni pamoja na:

i) Taasisi za Serikali;

ii) Taasisi za Elimu;

iii) Taasisi za Kitaaluma;

iv) Vyama vya Siasa;

v) Asasi za Kiraia (Civil Society Organizations) ikiwemo Jumuiya na Vyama vya Watu wenye Mahitaji Maalum, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (Non-Governmental Organizations) na Asasi za Kijamii (Community Based Organizations);

vi) Wadau wa Maendeleo;

vii) Vyombo vya Habari; na

viii) Wananchi Wapiga Kura.

### 3.8 Wajibu wa Wadau

Kila mdau atakayepata kibali cha kutoa Elimu ya Mpiga Kura atakuwa na wajibu wa:

i) Kujitambulisha katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri husika kabla ya kuanza zoezi la kutoa Elimu ya Mpiga Kura;

ii) Kuheshimu na kuzingatia Sheria za nchi;

iii) Kutumia kwa usahihi Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura uliotolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI;

iv) Kuzingatia masharti ya usajili;

v) Kuwa mzalendo, kuheshimu na kulinda maslahi ya nchi na utamaduni wa Mtanzania;

vi) Kutambua makundi maalum katika jamii wakati wa utoaji elimu;

vii) Kuweka wazi taarifa za mapato na matumizi ya fedha zitakazotumika na zilizotumika kutoa Elimu ya Mpiga Kura;

viii) Kuhakikisha anatoa elimu katika eneo na muda alioruhusiwa;

ix) Kuomba ufafanuzi kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI endapo kuna suala ambalo hajalielewa vema;

x) Kutoa fursa ya kuulizwa maswali na kuyajibu kwa ufasaha; na

xi) Kutoa taarifa ya maandishi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu mafanikio, changamoto na mapendekezo kuhusiana na zoezi zima la utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura.

### 3.9 Mambo Yasiyoruhusiwa Kufanywa na Wadau wa Elimu ya Mpiga Kura

Mambo ambayo hayapaswi kufanywa na wadau wanaohusika na kutoa Elimu ya Mpiga Kura ni pamoja na haya yafuatayo:

i) Kutumia mwongozo mwingine wa kufundishia zaidi ya ule uliotolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI;
ii) Kutoa Elimu ya Uraia badala ya Elimu ya Mpiga Kura;
iii) Kuhusisha Elimu ya Mpiga Kura na ushabiki wa kisiasa au itikadi za vyama vya siasa;
iv) Kutoa elimu inayolenga kuwagawa wananchi katika misingi ya dini, rangi, makabila, jinsia, maeneo na ulemavu;
v) Kujihusisha na vitendo vya rushwa na mambo yasiyoendana na maadili ya Mtanzania; na
vi) Kukasimu kazi ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa taasisi nyingine ambayo haikupewa kibali cha kufanya kazi hiyo.

### 3.10 Njia Zinazotumika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Elimu ya Mpiga Kura itatolewa kwa kutumia njia zifuatazo:

i) Mikusanyiko rasmi ya watu;
ii) Mikutano;
iii) Vipindi vya redio na runinga;
iv) Makala;
v) Sanaa za maonesho;
vi) Mitandao ya kijamii;
vii) Magari ya matangazo; na
viii) Machapisho ya vijitabu, vijarida, vipeperushi, mabango na mavazi yenye ujumbe kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

### 3.11 Makundi Maalum

Katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kuna makundi maalum ambayo ni muhimu kuyafikia na kuyapatia elimu inayohusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuhakikisha uwakilishi wa pande zote na kujenga jamii yenye usawa na maendeleo endelevu. Elimu ya Mpiga Kura itatolewa kwa kuzingatia mahitaji ya makundi maalum ambayo yanahitaji mkakati maalum ili kuyafikia. Vifaa na njia zitakazotumika kutoa elimu hiyo vitazingatia uwepo wa makundi hayo ili kuhakikisha kunakuwa na usawa katika kutoa elimu husika. Makundi maalum yamebainishwa kama ifuatavyo:

#### 3.11.1 Watu Waliojitenga kwa Sababu za Kijiografia na Shughuli za Kiuchumi

Kundi hili linajumuisha watu waliojitenga kwa sababu za kijiografia na shughuli za kiuchumi ambao wanaishi katika maeneo ya mbali, yasiyo na miundombinu rafiki ya usafiri au mawasiliano, na mara nyingi wanajihusisha na shughuli za kilimo, ufugaji, uwindaji au uvuvi. Kundi hili linauwezo wa kuleta mtazamo wa kipekee katika mchakato wa uchaguzi kutokana na uzoefu wao wa moja kwa moja katika changamoto za maisha ya vijijini.

Hata hivyo, kundi hili linakabiliwa na changamoto ya miundombinu ya usafiri, umbali mrefu kutoka vituo vya kupigia kura, ukosefu wa miundombinu ya mawasiliano na vifaa vya mawasiliano, kama vile simu za kisasa pamoja na kuwa na lugha zisizokuwa rasmi ambazo hazitumiki sana katika mawasiliano rasmi au mifumo ya elimu. Mikakati inayoweza kutumika katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa kundi hili ni kama ifuatavyo:

i) Kutumia njia za mawasiliano zinazofikika katika maeneo yao kama vile redio za jamii, au mikutano ya hadhara. Hii itawawezesha kupata habari kwa urahisi na kuwapa fursa ya kujifunza kuhusu mchakato wa uchaguzi;

ii) Ushirikishwaji wa viongozi wa kimila na wazee wenye ushawishi: Viongozi wa kijamii katika maeneo haya wanaweza kuwa na ushawishi mkubwa kwa wananchi;

iii) Kuanzisha vituo vya Elimu ya Mpiga Kura katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi ili kuliwezesha kundi hili kupata habari, kuuliza maswali, na kujadiliana kuhusu masuala ya uchaguzi;

iv) Kuhakikisha habari na mawasiliano yanatolewa kwa lugha wanayoielewa vizuri na kwa njia inayolingana na tamaduni zao.

### 3.11.2 Watu Wenye Ulemavu

Kundi hili linajumuisha wenye uoni hafifu, wasio sikia, wenye ulemavu wa ngozi na wenye ulemavu wa viungo. Ushiriki na uwakilishi wa watu wenye ulemavu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaweza kusaidia katika uundaji wa sera na programu zinazowalenga na kuhakikisha kuwa mahitaji yao yanazingatiwa. Hata hivyo, kundi hili linakabiliwa na changamoto ya upatikanaji mdogo wa miundombinu inayofaa pamoja na unyanyapaa na ubaguzi katika baadhi ya jamii kutokana na mila potofu. Mikakati ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura inayoweza kuimarisha ushiriki wa kundi hili inajumuisha mambo yafuatayo:

i) Kuandaa na kutumia vifaa vya elimu vinavyoweza kueleweka na watu wenye ulemavu mfano matumizi ya lugha za alama, nukta nundu, na teknolojia na mifumo ya mawasiliano inayoweza kutumiwa na watu wenye ulemavu;

ii) Kuwatumia watu wenye ushawishi miongoni mwao;

iii) Kuruhusiwa kwenda kituoni na wasaidizi wao na kupewa kipaumbele wafikapo kituoni;

iv) Kuhakikisha vituo vya kupigia kura vinakidhi mahitaji yao; na

v) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa uchaguzi kuhusu jinsi ya kushughulikia mahitaji yao kwa haki na usawa.

### 3.11.3 Wasiojua Kusoma na Kuandika

Kundi la watu wasiojua kusoma na kuandika linajumuisha watu ambao hawana ujuzi wa kimsingi wa kusoma na kuandika katika lugha yoyote. Kundi hili mara nyingi hutumia maarifa na hekima za kijadi katika kuleta mabadiliko chanya na maendeleo katika jamii zao. Hata hivyo, kundi hili linakabiliwa na changamoto ya kutambua, kuelewa, kutumia, kutafakari, na kushiriki katika shughuli za maandishi zinazohitajika kwa maisha ya kila siku. Mikakati ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa kundi hili inaweza kujumuisha matumizi ya njia za mawasiliano zisizo za maandishi kama vile mihadhara ya moja kwa moja, picha na sauti kwenye redio au televisheni za jamii, michezo au mijadala inayoshirikisha ushiriki wa moja kwa moja wa washiriki, mabango, nembo, na alama zenye ujumbe rahisi na wa kuvutia.

### 3.11.4 Wanawake

Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 ni miongoni mwa sera zinazolenga kuhakikisha kuwa wanawake wanapata fursa sawa katika nyanja zote za maisha na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ushiriki wa kundi la wanawake katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaweza kuleta mtazamo mpya na sauti za kipekee katika maamuzi ya kisiasa, huku wakileta ujuzi na uzoefu wao kutoka katika maisha yao ya kila siku, na kuwaunganisha wanajamii wenzao kushiriki katika mchakato wa uchaguzi. Hata hivyo, kundi hili linakabiliwa na changamoto za ubaguzi wa kijinsia, ukosefu wa rasilimali, ukatili na unyanyasaji, majukumu ya kifamilia na ukosefu wa fursa za elimu, ambazo zinaweza kuwazuia kushiriki kikamilifu katika mchakato huo. Hivyo, mikakati inayoweza kuimarisha ushiriki wa wanawake katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

i) Kuendeleza programu za elimu ambazo zinazingatia masuala ya kijinsia na yanayohusiana na wanawake, kama vile umuhimu wa uwakilishi wa wanawake katika Serikali za Mitaa;

ii) Kutoa mafunzo na vifaa vinavyowawezesha wanawake kushiriki katika mchakato wa uchaguzi, kama vile stadi za uongozi na ujasiri wa kisiasa;

iii) Kuanzisha mikakati ya kijamii na kiuchumi ambayo inawawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika siasa, kama vile kutoa huduma za utunzaji wa watoto wakati wa mikutano au kampeni;

iv) Kuelimisha umma kuwapisha wanawake wajawazito katika foleni ya uandikishaji au kupiga kura.

**3.11.5 Vijana**

Kundi la vijana pia ni moja ya makundi maalum katika muktadha wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kutokana na uwezo wao wa uvumbuzi na ubunifu, ujuzi wao wa teknolojia, na shauku yao ya kuleta mabadiliko katika taifa. Vijana wanaweza kuleta mbinu mpya za kutoa Elimu ya Mpiga Kura na kutumia zana za kidijitali kwa ufanisi katika kufikia wapiga kura. Hata hivyo, kundi hili linakabiliwa na changamoto za uwezekano mdogo wa kushiriki katika maamuzi ya kijamii, ubaguzi wa kijinsia, ukosefu wa rasilimali kama fedha na mtandao. Kwa kuzingatia fursa na changamoto hizi ni muhimu kuweka mikakati maalum ili kuhakikisha ushiriki wa vijana katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:

i) Kutoa elimu kupitia njia wanazopenda, kama vile matumizi ya teknolojia na mitandao ya kijamii, matamasha ya muziki, ngoma za asili na mihadhara rasmi;

ii) Kuchagua vijana wenye ushawishi katika jamii zao kama mabalozi wa kutoa Elimu ya Mpiga Kura. Vijana hawa wanaweza kuwa na uwezo wa kufikia vijana wenzao kwa njia inayoeleweka na inayovutia;

iii) Kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kuheshimu na kusikiliza maoni ya vijana katika mchakato wa uchaguzi na kuhakikisha kuwa fursa sawa za ushiriki zinapatikana kwa vijana wote, bila kujali jinsia, kabila au hali ya kiuchumi;

iv) Kutoa fursa za kujitolea katika kampeni na kuhamasisha vijana kushiriki katika mijadala ya kisiasa.

### 3.11.6 Wazee

Wazee ni kundi maalum katika uchaguzi wa serikali za mitaa kutokana na hekima, umri na uzoefu wao, ambao wanaweza kuleta maono ya muda mrefu na ufumbuzi wenye busara kwa changamoto za kijamii. Ushiriki wao pia unahakikisha uwakilishi wa vizazi vyao na wanaweza kutumia ushawishi wao kuhamasisha jamii kushiriki katika uchaguzi. Hata hivyo, wanakabiliwa na changamoto za kiafya, ubaguzi wa kijamii, ukosefu wa elimu na rasilimali. Kwa kuzingatia fursa na changamoto hizi ni muhimu kuwa na mkakati maalum ili kuhakikisha ushiriki wa wazee katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mikakati inayoweza kutumika ni pamoja na ifuatayo:

i) Kuwahusisha wazee wenye uzoefu na maarifa kusaidia katika kutoa elimu ya mpiga kura;

ii) Kuandaa mafunzo na mikutano maalum kwa wazee ili kuwaelimisha kuhusu mchakato wa uchaguzi na umuhimu wa ushiriki wao katika kupiga kura;

iii) Kutoa elimu kwa lugha na mbinu zinazoeleweka kwa wazee, kuzingatia uzoefu na uelewa wao wa kimatendo. Kwa mfano, badala ya kutumia lugha ya kiufundi ambayo inaweza kuwa ngumu kueleweka, waelimishaji wanaweza kutumia lugha rahisi na ya moja kwa moja, pamoja na mifano ya maisha halisi ili kusaidia wazee kuelewa mchakato wa uchaguzi;

iv) Kuhamasisha wazee kushiriki katika shughuli za uchaguzi kama vile kujisajili kupiga kura, kuhudhuria mikutano ya wagombea, na kupiga kura wakati wa siku ya uchaguzi;

v) Kufanya kazi kwa karibu na mamlaka za uchaguzi na jamii kuzuia ubaguzi na kuhakikisha kuwa wazee wanapata fursa sawa za kupiga kura na kushiriki katika mchakato wa uchaguzi. Mfano, kuweka vituo vya kujiandikisha na kupigia kura katika maeneo yanayofikika kwa urahisi kwa wazee na kutoa mafunzo kwa maafisa wa uchaguzi kuhusu kushughulikia mahitaji maalum ya wazee katika siku ya uchaguzi;

vi) Vilevile, kundi hili linatakiwa kupewa kipaumbele cha kutokaa katika mstari wakati wa kujiandikisha na kupiga kura siku ya uchaguzi.

### 3.11.7 Viongozi wenye Ushawishi katika Jamii

Hili ni kundi maalum katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa linalohusisha watu wenye ushawishi wanaounganisha na kuongoza jamii zao ambao wanaaminika na wanaheshimika kutokana na uwezo, uzoefu, maarifa na mchango wao katika maendeleo ya jamii. Hivyo, wanaweza kuwa na athari chanya katika kuhamasisha na kutoa elimu ya mpiga kura kwa sababu wananchi wanawasikiliza na kuwafuata. Mikakati inayoweza kutumika kutoa elimu ya mpiga kura kupitia viongozi wenye ushawishi katika jamii ni kama ifuatavyo:

1. Kuwezesha semina na warsha ambazo viongozi hawa wanaweza kushiriki ili kujifunza na kuelewa zaidi kuhusu mchakato wa uchaguzi na jinsi ya kutoa elimu kwa wanajamii wao;
2. Kuandaa mikutano na mihadhara ya hadhara ambapo viongozi hawa wanaweza kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kupiga kura na mchakato wa uchaguzi;
3. Kuweka matangazo kwenye redio, runinga, na mitandao ya kijamii ambapo viongozi hawa wanaweza kusambaza ujumbe wa elimu kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**Maswali:**

1. Ni wadau gani wanapaswa kupewa Elimu ya Upigaji Kura?
2. Ni mambo gani hayapaswi kufanywa na Wadau wakati wa kutoa elimu ya mpiga kura?

3. Taja njia zinazotumika kutoa elimu ya mpiga kura.
4. Ni vigezo gani vinavyotumika katika kutoa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura?
5. Njia zipi zinafaa kutumika kutoa elimu ya mpiga kura kwa makundi maalum?

# SURA YA NNE

# UANDIKISHAJI NA UANDAAJI WA ORODHA YA WAPIGA KURA

## 4.1 Utangulizi

Mwananchi anaandikishwa kwenye orodha ya wapiga kura ili aweze kuwa na sifa ya kupiga kura. Uandikishaji wapiga kura ufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Mji) Sura 288 na Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2024, Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2024, na Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2024, Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo za Mwaka 2024.

Sura hii inalenga kubainisha masuala yanayohusu uandikishaji wapiga kura na uandaaji wa orodha ya wapiga kura. Hivyo, sura hii itamwezesha mwananchi kuelewa kuhusu: sifa za mpiga kura; kupoteza sifa ya kupiga kura; uteuzi wa waandikishaji na waandaaji wa orodha ya wapiga kura; muda wa uandikishaji wapiga kura; uhakiki wa orodha ya wapiga kura; mawakala wa uandikishaji wa wapiga kura; pingamizi kuhusu uandikishaji na fomu zinazotumika katika uchaguzi.

### 4.2 Sifa za Kuandikishwa katika Orodha ya Wapiga Kura

Mkazi yeyote atakuwa na haki ya kuandikishwa kupiga kura endapo atakuwa na sifa zifuatazo:

i) Ni raia wa Tanzania;

ii) Ana umri wa miaka kumi na nane au zaidi ifikapo siku ya uchaguzi;

iii) Ni mkazi wa eneo la kitongoji au mtaa husika; na

iv) Ana akili timamu.

Mwananchi ambaye atakosa sifa mojawapo kati ya zilizoainishwa katika kipengele cha 4.2 anaweza kuwekewa pingamizi.

### 4.3 Mahali na Muda wa Uandikishaji Wapiga Kura

i) Uandikishaji na uandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura utaanza siku ya arobaini na saba (47) kabla ya siku ya uchaguzi;

ii) Uandikishaji utafanyika kwa muda wa siku kumi (10) kwa kutumia fomu zilizoanishwa katika Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2024;

iii) Uandikishaji utafanyika katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa ameshauriana na Viongozi wa Vyama vya Siasa lakini maamuzi ya mwisho yatakuwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi;

iv) Vituo vya uandikishaji wa wapiga kura vitafunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni; na

v) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika matangazo ya uchaguzi na Orodha ya Wapiga Kura siku moja baada ya kukamilika kwa uandikishaji wa wapiga kura na atatunza orodha halisi.

### 4.4 Uhakiki wa Orodha ya Wapiga Kura

Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura atakuwa na haki ya kukagua Orodha ya Wapiga Kura katika muda wa siku saba (7) tangu tarehe ya orodha hiyo kubandikwa ili:

i) Kuomba kurekebisha jina lake kwa herufi, kuongeza au kupunguza;

ii) Kuomba kubadilisha taarifa zilizoko katika orodha hiyo;

iii) Kuomba kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki; na

iv) Kuweka pingamizi kuhusu usahihi wa orodha hiyo.

**4.5 Uteuzi wa Waandikishaji na Waandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura**

i) Waandikishaji na waandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura watateuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi siku hamsini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi; na

ii) Watendaji wa Kata na Vijiji hawataruhusiwa kuteuliwa kuwa waandikishaji au waandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura.

**4.6 Mawakala wa Uandikishaji wa Wapiga Kura**

Chama cha Siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa Sura 258 kitaruhusiwa kuteua wakala wake kwa kila kituo cha uandikishaji wa wapiga kura wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

**4.7 Pingamizi kuhusu Uandikishaji**

i) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura anaweza kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura kabla ya kumalizika kwa muda wa kukagua Orodha ya Wapiga Kura;

ii) Pingamizi litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atatakiwa kutoa uamuzi kuhusu pingamizi lililowekwa ndani ya siku mbili (2) tangu tarehe ya mwisho ya ukaguzi wa Orodha ya Wapiga Kura;

iii) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi akiridhika na pingamizi lililowekwa, atarekebisha Orodha ya Wapiga Kura iliyotangazwa baada ya muda wa siku mbili (2) isipokuwa kama uamuzi wake umekatiwa rufaa;

iv) Mtu aliyeweka au aliyewekewa pingamizi asiporidhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi lililowasilishwa kwake, atawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ndani ya muda wa siku mbili (2) tangu kutolewa kwa uamuzi wa pingamizi;

v) Msimamizi wa Uchaguzi, atashughulikia rufaa iliyowasilishwa kwake na kutoa uamuzi ndani ya siku nne (4) tangu siku ya kupokea rufaa hiyo; na

vi) Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa hiyo utakuwa wa mwisho.

### 4.8 Fomu zitakazotumika katika Zoezi la Uandikishaji wa Wapiga Kura

Katika zoezi la uandikishaji wa wapiga Kura, Fomu zitakazotumika ni Fomu ya Orodha ya Wapiga Kura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**Maswali**

i) Taja sifa za mtu kuandikishwa katika Orodha ya Wapiga Kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa?

ii) Taja sababu zinazo mkosesha mtu sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa?

iii) Eleza umuhimu wa kubandika Orodha ya Wapiga Kura kwenye vituo vya kujiandikishia?

iv) Taja sababu za mtu kuwekewa pingamizi?

v) Taja haki za mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Mpiga kura

## SURA YA TANO

## UTEUZI, PINGAMIZI NA RUFAA ZA WAGOMBEA

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kuonesha sifa za mgombea; muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi; utaratibu wa uteuzi wa mgombea; utaratibu wa uteuzi wa mgombea pekee; kupoteza sifa ya kuwa mgombea; pingamizi dhidi ya mgombea; taratibu za kushughulikia rufaa; kifo cha mgombea; na utaratibu wa mgombea kujitoa katika uchaguzi.

### 5.2 Sifa za Mgombea

Katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mkazi yeyote wa Kitongoji au Mtaa anaweza kugombea Uenyekiti wa Kijiji, Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji, Uenyekiti wa Kitongoji katika Kijiji au Mamlaka ya Mji Mdogo, Uenyekiti wa Mtaa na Ujumbe wa Kamati ya Mtaa endapo atakuwa na sifa zifuatazo:

i) Ni raia wa Tanzania;
ii) Ana umri wa miaka ishirini na moja au zaidi;
iii) Ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
iv) Ana shughuli halali ya kiuchumi ya kumwezesha kuishi;
v) Ni mkazi wa eneo husika;
vi) Ni mwanachama wa Chama cha Siasa na amedhaminiwa na Chama hicho; na
vii) Awe na akili timamu.

### 5.3 Kukosa Sifa ya Kuwa Mgombea

Mtu hatakuwa na sifa za kugombea endapo:

i) Amepoteza au hana sifa za mgombea zilizoainishwa katika sehemu ya 5.2;
ii) Ana mkataba au maslahi kwenye kampuni ambayo ina mkataba na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo anagombea nafasi ya uongozi na hajatangaza kuwepo

kwa mkataba au maslahi yake kupitia kwenye gazeti linalopatikana katika eneo husika au mbao za matangazo katika ofisi ya kijiji au mtaa;

iii) Amepoteza sifa ya kupiga kura kwa mujibu wa kanuni ; na

iv) Ataajiriwa au kuteuliwa katika wadhifa wowote katika Utumishi wa Umma au kuchaguliwa katika nafasi ya udiwani, ubunge, Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Umakamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 5.4 Muda wa Kuchukua na Kurudisha Fomu za Uteuzi

Mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi yoyote katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa atatakiwa kuchukua fomu ya uteuzi siku zisizopungua ishirini na sita (26) kabla ya siku ya uchaguzi.

Muda wa kurejesha fomu utakuwa siku saba (7) tangu siku ya kwanza ya kuchukua fomu iliyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi. Fomu zitatolewa na kupokelewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

### 5.5 Utaratibu wa Uteuzi wa Wagombea

Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi:

i) Atateua wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji, ujumbe wa Kamati ya Mtaa na uenyekiti wa Kitongoji katika kijiji au Mamlaka ya Mji Mdogo siku kumi na tisa (19) kabla ya tarehe ya uchaguzi;

ii) Atabandika fomu za maombi ya uteuzi za wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea;

iii) Endapo mgombea ataomba kujitoa katika uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi wa mgombea huyo na wagombea waliobaki watapigiwa kura ili kupata mshindi;

iv) Atatoa taarifa kwa vyama vya siasa na wakazi wa Kijiji/Mtaa au Kitongoji kuhusu kukosekana kwa waombaji au kutokuwepo kwa waombaji wenye sifa endapo itatokea hivyo; na

v) Atatoa taarifa kwa vyama vya siasa na wakazi wa eneo husika kuhusu kurudiwa kwa mchakato wa uchaguzi baada ya siku arobaini kuanzia tarehe ya uteuzi.

**5.6 Utaratibu wa Uteuzi wa Mgombea Pekee**

i) Endapo siku ya uteuzi kutakuwa na mwombaji mmoja pekee aliyekidhi vigezo katika nafasi inayogombewa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamteua mwombaji huyo kuwa mgombea pekee kwa nafasi aliyoomba;

ii) Endapo idadi ya waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa au Halmashauri ya Kijiji, wenye sifa itakuwa sawa na idadi ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawateua waombaji hao kuwa wagombea pekee kwa nafasi waliyoomba;

iii) Endapo idadi ya waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya mtaa au Halmashauri ya Kijiji, wenye sifa itakuwa chini ya idadi ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawateua waombaji hao kuwa ni wagombea pekee wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Mtaa.

**5.7 Pingamizi Dhidi ya Wagombea**

Mgombea ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kuwasilisha pingamizi kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili (2) tangu uamuzi au uteuzi ulipofanyika, na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili (2) kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.

**5.8 Taratibu za Kushughulikia Rufaa**

Mwombaji au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufani iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kanuni katika muda usiozidi siku nne (4) kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi. Kamati ya Rufani baada ya

kupokea rufaa itatoa uamuzi wake ndani ya siku nne (4) kuanzia siku ya kupokea rufaa na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

### 5.9 Kifo kwa Mgombea

Iwapo mgombea atafariki, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha uchaguzi wa nafasi hiyo na Chama cha Siasa kilichotoa mgombea aliyefariki kinaweza kuwasilisha jina la mwombaji mwingine ndani ya siku arobaini tangu kuahirishwa kwa uchaguzi ili hatua za uteuzi wa mwombaji huyo zifanyike.

### 5.10 Kujitoa kwa Mgombea

Mgombea atajitoa kwenye uchaguzi kwa kujaza fomu maalumu kwa mujibu wa kanuni. Aidha, mgombea mwenye kusudio la kujitoa atatakiwa kufanya hivyo ndani ya kipindi cha siku nne (4) tangu tarehe ya uteuzi. Mgombea akikamilisha taratibu za kujitoa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi wa mgombea huyo na wagombea waliobaki watapigiwa kura ili kupata mshindi.

### 5.11 Fomu za Maombi ya Uteuzi

Mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi ya uongozi atatakiwa kujaza Fomu ya maombi ya uteuzi kugombea nafasi husika kwa mujibu wa Kanuni.

**Maswali**

1. Taja zifa za mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji/Kitongoji/Mtaa.
2. Taja sifa za wajumbe wa Serikali ya Kijiji/Mtaa.
3. Taja sababu zinazopelekea mgombea kupoteza sifa.
4. Nani anaruhusiwa kumwekea pingamizi mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji/Kitongoji/Mtaa?
5. Taja sababu na muda unaoruhusiwa kwa mtu kuwekewa pingamizi.
6. Taja taratibu mbalimbali za kushughulikia rufaa.
7. Elezea taratibu za uteuzi, pingamizi na rufaa zinazotumika pale inapotokea kuna Mgombea Pekee.

# SURA YA SITA

# KAMPENI ZA UCHAGUZI

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kuelezea taratibu za kampeni za uchaguzi, mambo muhimu ya kuzingatiwa, wajibu wa wadau mbalimbali watakaohusika katika kampeni za uchaguzi na taratibu za maadili katika kipindi chote cha kampeni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hivyo, sura hii itamwezesha mwananchi kuelewa kuhusu: ratiba ya kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; wajibu wake katika kampeni za uchaguzi; maadili yanayopaswa kuzingatiwa na wadau wa uchaguzi wakati wa kampeni; na utaratibu wa kufuata katika kushugulikia malalamiko wakati wa kampeni.

## 6.2 Mambo Muhimu ya Kuzingatia

Wananchi na wadau wa uchaguzi watapaswa kuzingatia masuala yafuatayo wakati wa kampeni za uchaguzi:

i) Kampeni za Uchaguzi zitafanyika siku saba (7) kabla ya siku ya Uchaguzi;

ii) Mikutano ya kampeni za uchaguzi itaanza saa mbili kamili asubuhi na itamalizika saa kumi na mbili kamili jioni ya kila siku ya kampeni;

iii) Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si chini ya siku saba kabla ya kuanza kwa kampeni;

iv) Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba ya kampeni za Uchaguzi kwa kushirikisha vyama vya siasa vitakavyoshiriki Uchaguzi. Iwapo vitashindwa kuridhiana, Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni na uamuzi wake utakuwa wa mwisho;

v) Msimamizi wa Uchaguzi atawasilisha ratiba ya kampeni za uchaguzi kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Wilaya ambaye atakuwa na wajibu wa kuisimamia ili kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwepo kwa kipindi chote cha kampeni. Aidha, atavipatia Vyama vya Siasa nakala ya ratiba hiyo; na

vi) Ratiba ya Kampeni itakayowasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya itakuwa ni taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni.

### 6.3 Wajibu wa Wadau wa Uchaguzi Wakati wa Kampeni

Wadau mbalimbali wa uchaguzi watakuwa na wajibu ufuatao:

#### 6.3.1 Jeshi la Polisi

i) Kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwepo katika mikutano ya kampeni;

ii) Kuhakikisha mikutano ya kampeni za Uchaguzi inafanyika kwa kuzingatia ratiba ya kampeni; na

iii) Ulinzi wa raia na mali zao.

#### 6.3.2 Msimamizi wa Uchaguzi

i) Kuitisha kikao na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki Uchaguzi ili kujadili maombi ya mabadiliko ya ratiba; na

ii) Kuwasilisha mabadiliko ya ratiba yaliyokubaliwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya kwa ajili ya kupatiwa ulinzi siku ya mkutano wa kampeni.

#### 6.3.3 Chama cha Siasa

i) Kuendesha mikutano ya kampeni za Uchaguzi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, miongozo na ratiba ya uchaguzi;

ii) Kuwasilisha kwa maandishi mapendekezo ya mabadiliko ya ratiba ya Kampeni kwa Msimamizi wa Uchaguzi pale inapobidi na kuyatekeleza baada ya kuridhiwa; na

iii) Kuendesha kampeni za uchaguzi bila kujihusisha na vitendo vya rushwa; kutoa maneno ya kashfa au lugha za matusi; kufanya ubaguzi wa jinsia, ulemavu, dini, rangi, hali ya uchumi wa mtu au jamii, kabila, itikadi au ubaguzi mwingine wa aina yoyote au kutoa maneno ambayo yanaweza kusababisha vurugu au uvunjifu wa amani.

#### 6.3.4 Wananchi

Wananchi watakuwa na wajibu wa kufanya mambo yafuatayo:

i) Kutii Sheria, Kanuni na Miongozo ya Uchaguzi;

ii) Kushiriki mikutano ya kampeni;

iii) Kutojihusisha na vitendo vya rushwa;

iv) Kutofanya vitendo vya uvunjifu wa amani; na

v) Kuhoji na kuuliza maswali endapo hawajaelewa.

### 6.4 Taratibu za Maadili

Wadau wa Uchaguzi watazingatia taratibu za maadili ya uchaguzi kama ifuatavyo:

#### 6.4.1 Vyama vya Siasa

Vyama vya Siasa havipaswi kufanya yafuatayo:

i) Kusababisha au kufanya fujo au vurugu ya aina yoyote katika Mkutano wake au wa Chama kingine;

ii) Kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, dini, rangi na aina za ulemavu kwenye mikutano ya kampeni;

iii) Kukataza wanachama au wafuasi kutamka kauli mbiu, kuonesha ishara za Vyama vyao, au kuvaa sare zenye rangi ya Chama chao katika mikutano ya hadhara ya Vyama vingine;

iv) Kubeba sanamu, kinyago au kitu chochote ambacho kinaonyesha kudhalilisha, kukebehi, kufedhehesha au kukejeli Chama kingine cha Siasa au Mgombea au Kiongozi wa Chama kingine cha Siasa au Serikali katika mkutano wowote wa kampeni za Uchaguzi;

v) Kutumia vipaza sauti vya aina yoyote kwa shughuli za kisiasa mara baada ya muda wa kampeni za uchaguzi kumalizika;

vi) Kuchafua, kubandua, kuchoma au kuharibu, kwa namna yoyote ile matangazo ya kampeni ya Vyama vingine vya Siasa na matangazo mengine yanayotolewa na Mamlaka za Uchaguzi;

vii) Kubandika mabango ya kampeni, matangazo au mchoro wowote kwenye nyumba, majengo au vyombo vya usafiri vya watu binafsi au taasisi mbalimbali bila idhini ya wamiliki husika;

viii) Kubandika mabango ya kampeni, matangazo au mchoro wowote kwenye nyumba za ibada, taasisi za dini, taasisi binafsi zinazohudumia umma, majengo ya Serikali na taasisi zake;

ix) Kutoa rushwa ili kumshawishi mtu yeyote kupiga kura, kugombea au kujitoa katika kugombea nafasi ya uongozi;

x) Kuzuia mtu yeyote, watu au wafuasi wa vyama vingine kuhudhuria mikutano ya kampeni au kupiga kura;

xi) Kukodi au kutumia usafiri wa aina yoyote kubeba na kusafirisha wapiga kura kwa madhumuni ya kushawishi kupigiwa kura;

xii) Kuacha mabango, matangazo na machapisho ya aina yoyote ile yaliyotumika wakati wa kampeni katika sehemu za wazi ~~baada ya~~ baada ya Uchaguzi; na

xiii) Kuhamasisha na kushawishi wanachama au wafuasi kupiga kura zaidi ya mara moja.

**6.4.2 Serikali**

Serikali itakuwa na Wajibu wa:

(i) Kutoa fursa sawa kwa wadau wote wa Uchaguzi hususani Vyama vya Siasa na Wagombea ili kuendesha shughuli zao za kisiasa wakati wa Uchaguzi kwa uhuru na kuzingatia Sheria za nchi;

(ii) Kuhakikisha hali ya usalama, amani na utulivu wakati wote wa Uchaguzi; na

(iii) Kuhakikisha kuwa viongozi na watendaji wake wanazingatia ipasavyo ukomo wa madaraka yao katika shughuli za Uchaguzi.

### 6.4.3 Wasimamizi wa Uchaguzi

Wasimamizi wa Uchaguzi watawajibika kuzingatia yafuatayo:

i) Kusimamia uchaguzi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na weledi; na

ii) Kutofanya upendeleo wa aina yoyote; na

iii) Kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

## 6.5 Kamati za Maadili ya Uchaguzi

Kutakuwa na Kamati za Maadili zitakazoundwa na Msimamizi wa Uchaguzi kama ifuatavyo:

### 6.5.1 Kamati ya Maadili ya Halmashauri

Kamati ya Maadili ya Halmashauri itakuwa na wajumbe wafuatao:

i) Msimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;

ii) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi katika Halmashauri;

iii) Mjumbe mmoja atakayewakilisha Serikali ambaye atateuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na

iv) Afisa Uchaguzi ambaye atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi.

### 6.5.2 Kamati ya Maadili Ngazi ya Kata

Kamati ya Maadili Ngazi ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:

i) Msimamizi Msaidizi ngazi ya Kata husika ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;

ii) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki katika Uchaguzi kwenye Kata;

iii) Mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na

iv) Katibu ambaye ni Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kijiji/ mtaa atakayeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

**6.6 Rufaa Dhidi ya Maamuzi**

i) Upande ambao hautaridhika na uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata, utakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Kamati ya Maadili ya Halmashauri ndani ya siku mbili (2) tangu uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata ulipotolewa; na

ii) Kamati ya Maadili ya Halmashauri itatoa maamuzi ya rufaa husika mapema iwezekanavyo na uamuzi huo utakuwa ni wa mwisho.

**6.7 Malalamiko dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi**

i) Pale ambapo malalamiko yaliyowasilishwa dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili`ya Uchaguzi, Msimamizi au Msimamizi Msaidizi, Msimamizi wa Uchaguzi hataendesha Kikao hicho, isipokuwa Katibu Tawala wa Mkoa atateua Afisa yeyote wa Umma Mwandamizi kutoka Sekretarieti ya Mkoa kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho; na

ii) Iwapo Kamati itaona kuwa Msimamizi amekosea Kamati itamtaka Msimamizi wa Uchaguzi kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**6.8 Uwasilishwaji wa Malalamiko ya Ukiukwaji wa Maadili**

Mgombea yeyote, Wasimamizi wa Uchaguzi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, Serikali au Chama chenye mgombea kinachoamini kwamba Maadili ya Uchaguzi yamekiukwa kitawasilisha malalamiko kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Kata kwa maandishi ndani ya siku tatu (3) tangu kutokea kwa tukio linalolalamikiwa.

**Maswali**

1. Taja wajibu wa Serikali katika uchaguzi?
2. Nini wajibu wa mwananchi katika kampeni za uchaguzi?
3. Ni mambo gani yasiyoruhusiwa wakati wa Kampeni za uchaguzi?
4. Ni zipi taratibu za kushughulikia malalamiko wakati wa Kampeni za uchaguzi?
5. Taja wajumbe wa Kamati ya maadili?
6. Nini kazi ya kamati za maadili?

# SURA YA SABA

# TARATIBU ZA UPIGAJI KURA

## 7.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kutoa maelezo kuhusu sifa za mpiga kura, mahali, vituo na muda wa kupiga kura, masanduku ya kura, karatasi zitakazotumika wakati wa kupiga kura, utaratibu utakaozingatiwa wakati wa kupiga kura, usaidizi kwa wenye mahitaji maalum, mambo ya kuzingatia wakati wa kupiga kura na watu wanaoruhusiwa kuwepo kwenye kituo cha kupigia kura.

## 7.2 Sifa za Mpiga Kura

Mpiga kura anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

i) Ni raia wa Tanzania;

ii) Ana umri wa miaka kumi na nane au zaidi ifikapo siku ya uchaguzi;

iii) Ni mkazi wa eneo la Kitongoji/Mtaa;

iv) Ana akili timamu; na

v) Amejiandikisha kupiga kura katika Mtaa au Kitongoji husika.

## 7.3 Mahali, Vituo na Muda wa Kupiga Kura

Uchaguzi wa viongozi wa Serikali za Mitaa utafanyika katika vituo maalum vya kupigia kura ambavyo vitakuwa katika majengo ya umma yaliyopo katika Vitongoji au Mitaa husika. Endapo Kitongoji au Mtaa hauna majengo ya umma, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kushauriana na wagombea au vyama vya siasa vyenye wagombea atateua eneo lingine kuwa kituo cha kupigia kura.

Kura zitapigwa kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni. Baada ya saa kumi kamili Askari atakaa nyuma ya Mpiga kura wa mwisho ili kuzuia watu waliochelewa kufika kituoni kupiga kura.

### 7.4 Masanduku ya Kura

Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi wa Kituo atawaonesha wapiga kura masanduku maalum ya kupigia kura yaliyotengenezwa kwa namna itakayomwezesha Mpiga kura kutumbukiza kura zake kwa urahisi kwa kila nafasi itakayopigiwa kura, masanduku yatakuwa wazi na atayafunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

### 7.5 Karatasi za Kupigia Kura

Kura zitapigwa kwa kutumia karatasi maalum za kupigia kura zenye majina ya wagombea na vyama wanavyowakilisha.

### 7.6 Utambulisho wa Mpiga Kura

i) Kabla Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajampatia mpiga kura karatasi ya kupigia kura atajiridhisha kama jina la mpiga kura limeorodheshwa katika orodha ya wapiga kura;

ii) Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye Orodha ya Wapiga Kura;

iii) Mpiga kura anaweza kutakiwa kuonesha mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:

   (a) Kitambulisho cha mpiga kura;
   (b) Kitambulisho cha kazi;
   (c) Hati ya kusafiria;
   (d) Kadi ya bima ya afya;
   (e) Kitambulisho cha shule au chuo;
   (f) Kitambulisho cha mifuko ya hifadhi ya jamii;
   (g) Leseni ya udereva; au
   (h) Kitambulisho cha Taifa.

iv) Endapo mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote kati ya vilivyotajwa, lakini jina lake limo kwenye Orodha ya Wapiga Kura iliyoandaliwa

kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.

### 7.7 Upigaji Kura

i) Kura zitapigwa katika namna itakayozingatia usiri;

ii) Mpiga kura atapatiwa karatasi ya kupigia kura kulingana na idadi ya nafasi zinazogombewa;

iii) Mpiga kura ataweka alama ya **vema (√)** katika jina la mgombea anayemtaka;

iv) Kura ikishapigwa itakunjwa na kutumbukizwa katika sanduku maalum la kuhifadhia kura;

v) Baada ya kupiga kura, mpiga kura atatakiwa kuchovya kidole cha mkono katika kidau cha wino; na

vi) Mpiga kura atatakiwa kuondoka eneo la kupigia kura baada ya kupiga kura.

### 7.8 Usaidizi kwa Wenye Mahitaji Maalum

Mpiga kura ambaye kwa sababu ya ulemavu wa macho au ulemavu mwingine wowote; au hajui kusoma na kuandika, anaweza kumwomba mtu yeyote kumsaidia kupiga kura; isipokuwa mpiga kura huyo hataruhusiwa kuomba usaidizi wa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, mgombea au wakala wake. Mtu mmoja hataruhusiwa kumsaidia mpiga kura zaidi ya mmoja.

### 7.9 Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Kupiga Kura

i) Epuka kupiga kura kwa Mgombea zaidi ya mmoja katika nafasi moja;

ii) Weka alama ya vema katika kisanduku cha mgombea;

iii) Epuka kumpigia kura Mgombea aliyejitoa;

iv) Epuka kuharibu karatasi ya kupigia kura;

v) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kutumia simu ya kiganjani ndani ya kituo cha kuhesabu na kujumlisha kura isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi

Msaidizi wa Kituo na Mlinzi wa Kituo cha Kupigia Kura ambao watatumia simu zao pale inapobidi kwa shughuli za uchaguzi tu, na simu hizo wakati wote ziwekwe kwenye mtetemo.

### 7.10 Watu Wanaoruhusiwa Kuingia Kwenye Kituo cha Kupiga Kura

i) Msimamizi wa Uchaguzi;

ii) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

iii) Msimamizi wa Kituo;

iv) Wakala wa chama cha siasa chenye Mgombea;

v) Mpiga kura;

vi) Mtu anaye msaidia mpiga kura asiyeweza kupiga kura mwenyewe;

vii) Mwangalizi wa ndani wa uchaguzi aliyeruhusiwa kwa maandishi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

viii) Mgombea; na

ix) Askari/mgambo.

**Maswali**

1. Eleza utaratibu wa kupiga kura.
2. Je, unafahamu baada ya kupiga kura unatakiwa kufanya nini?
3. Je, ni vitambulisho gani mpiga kura atapaswa kuonesha mara baada ya Msimamizi wa kituo kumtaka kufanya hivyo?
4. Ni hatua zipi zinazopaswa kuchukuliwa na Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura ili kumruhusu mtu ambaye hana kitambulisho cha kura kupiga kura?
5. Taja Watu wanaohusika kuingia kwenye Kituo cha Kupigia Kura.

# SURA YA NANE

# KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

## 8.1 Utangulizi

Sura hii inatoa ufafanuzi kuhusu watu wanaopaswa kuwepo ndani ya kituo cha kuhesabu na kujumlisha kura, utaratibu wa zoezi la kuhesabu kura na kutangaza matokeo. Aidha, inabainisha maelezo kuhusu vituo vya kupigia kura na vifaa vinavyotumika wakati wa uchaguzi.

## 8.2 Wanaopaswa Kuwepo Wakati wa Kuhesabu Kura na Kujumlisha Matokeo

Wafuatao wataruhusiwa kuwepo ndani ya kituo na kushuhudia zoezi la kuhesabu kura na kujumlisha:

i) Msimamizi wa Uchaguzi;

ii) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

iii) Msimamizi wa Kituo;

iv) Wakala wa Mgombea;

v) Mgombea;

vi) Askari Polisi, Mgambo mwenye sare au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi; na

vii) Mwangalizi wa uchaguzi mwenye kitambulisho.

## 8.3 Kuhesabu Kura

Wakati wa kuhesabu kura yafuatayo yatafanyika:

i) Zoezi la kuhesabu kura litaanza baada ya kukamilika upigaji kura;

ii) Kituo cha kupigia kura kitageuka kuwa kituo cha kuhesabia kura;

iii) Kabla ya kuanza kuhesabu kura, Msimamizi wa Kituo atafanya yafuatayo:

   (a) atahakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;

   (b) atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;

   (c) atakagua lakiri na kuona kama haijafunguliwa;

(d) atakata lakiri; na

(e) Atafungua sanduku la kupigia Kura.

iv) Kura zitahesabiwa mbele ya wakala na/au mgombea

### 8.4 Sifa za Kura Zitakazokataliwa

Kura itachukuliwa kuwa imekataliwa iwapo:

i) Itakuwa na kitu au alama yoyote yenye kumtambulisha mpiga kura;

ii) Itakuwa imepigwa kwa mgombea aliyejitoa kwa mujibu wa sheria za uchaguzi;

iii) Alama imewekwa kwa mgombea zaidi ya mmoja na;

iv) Haina alama yoyote.

### 8.5 Kujumlisha na Kutangaza Matokeo

i) Kituo cha kuhesabia kura kitageuka kuwa kituo cha kujumlishia na kutangaza matokeo ya mwenyekiti wa kitongoji baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika;

ii) Kura za wagombea wa nafasi ya Uenyekiti wa Mtaa na Ujumbe wa Kamati ya Mtaa zitajumlishwa na matokeo kutangazwa katika kituo cha kujumlishia kura kitakachokuwa katika Ofisi ya Mtaa au mahali kwingine kadri Msimamizi wa Uchaguzi atakavyoelekeza;

iii) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea fomu za matokeo ya kura za nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kutoka kwa wasimamizi wa vituo vya kupigia kura, atajumlisha idadi ya kura kwa kila mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na kujaza matokeo katika fomu ya matokeo ya jumla na kutangazwa katika kituo cha kujumlishia kura kitakachokuwa katika Ofisi ya Serikali ya Kijiji au mahali kwingine kadri Msimamizi wa Uchaguzi atakavyoelekeza;

iv) Matokeo ya Uchaguzi yatajazwa kwenye Fomu Maalum ambayo itasainiwa na wagombea au wawakilishi wao pamoja na Msimamizi wa Kituo na kubandikwa kwenye sehemu ya Matangazo ya Uchaguzi;

v) Mgombea atakayepata kura nyingi kuliko wengine atatangazwa kuwa mshindi;

vi) Endapo idadi ya kura za wagombea waliopata kura nyingi kuliko wengine zitalingana, Msimamizi wa Uchaguzi atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uchaguzi; na

vii) Wakala au mgombea kutosaini au kukataa kusaini fomu ya matokeo au kutokuwepo kwenye kituo cha kuhesabu kura, kujumlisha na kutangaza matokeo, hakutosababisha kazi hiyo isifanyike na haitobatilisha matokeo.

Bila kuathiri maelezo yaliyotangulia, pale ambapo nafasi ya Wajumbe wa Kamati husika kupitia kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake na Wajumbe wa Kamati husika kupitia kundi la wanawake lina wagombea pekee, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea pekee kuwa Mjumbe wa Kamati husika kupitia kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake na Wajumbe wa Kamati husika kupitia kundi la wanawake endapo atakuwa amepata kura nyingi za NDIYO. Endapo idadi ya kura za NDIYO na HAPANA kwa Mjumbe wa Kamati husika kupitia kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake na Mjumbe wa Kamati husika kupitia kundi la wanawake zitalingana, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo hayo na kuwasilisha taarifa ya Uchaguzi huo kwa Msimamizi wa Uchaguzi ambaye atapanga tarehe nyingine ya Uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya Uchaguzi.

**Maswali**

i) Je ni hatua gani inayofuata baada ya zoezi la kupiga kura?

ii) Nani anaruhusiwa kuingia katika kituo cha kuhesabu kura, kujumlisha na kutangaza matokeo?

iii) Je, ni mazingira yapi humfanya mgombea pekee kutangazwa kushinda nafasi aliyogombea?

**iv)** Ni nini kitatokea endapo kura za NDIO na HAPANA kwa mgombea pekee zitalingana?

# SURA YA TISA

## MAWAKALA NA WAANGALIZI WA UCHAGUZI

### 9.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kuelezea maana, sifa na majukumu ya Wakala wa Vyama vya Siasa na Waangalizi wa Uchaguzi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

### 9.2 Wakala wa Vyama vya Siasa Kwenye Uchaguzi

Wakala wa Chama cha Siasa kwenye Uchaguzi ni mtu aliyeteuliwa na Chama na jina lake kuwasilishwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo atakula kiapo chini ya Hakimu, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

i) Chama cha Siasa chenye mgombea wa nafasi yoyote katika uchaguzi kinaweza kuteua wakala wake kwa kila kituo cha kupigia Kura ambaye atazingatia Sheria na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa;

ii) Wakala wa Chama cha Siasa atashuhudia zoezi la uandikishaji wa wapiga kura, kupiga kura, kujumlisha, kuhesabu na kutangaza matokeo; na

iii) Pia Wakala wa Chama cha Siasa atawajibika kufuata maadili yote ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa;

### 9.3 Vigezo vya kuwa Wakala wa Chama cha Siasa

Wakala wa Chama cha Siasa atapaswa kuwa na vigezo vifuatavyo:

i) Ameteuliwa na chama chake cha siasa;

ii) Awe na barua ya uteuzi kutoka chama kilichomteua;

iii) Ameapa kiapo cha kutunza siri;

iv) Ana miaka kumi na nane na kuendelea; na

v) Ana akili timamu.

### 9.4 Jukumu la Wakala wa Chama cha Siasa:

Wakala wa Chama cha Siasa atakuwa na majukumu yafuatayo:

i) Kutambua wapiga kura;

ii) Kulinda maslahi ya Chama na Mgombea anayemuwakilisha;

iii) Kushirikiana na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo na Msimamizi Msaidizi wa Kituo ili kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu zinazohusu upigaji, kuhesabu, kujumlisha kura na kutangaza matokeo zinafuatwa katika kituo;

iv) Kushuhudia zoezi la uandikishaji wa wapiga kura katika kituo cha kuandikisha wapiga kura; na

v) Kufuata maadili yote ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

### 9.5 Waangalizi wa Uchaguzi

i) Waangalizi wa uchaguzi ni waangalizi wa ndani wa uchaguzi wenye kibali cha Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

ii) Maombi ya kibali cha uangalizi wa uchaguzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya Tangazo la Uchaguzi kutolewa; na

iii) Waangalizi wa ndani wa uchaguzi watafanya shughuli za uangalizi kwa gharama zao wenyewe.

### 9.6 Vigezo vya kuwa Mwangalizi wa Ndani wa Uchaguzi

i) Iwe ni taasisi iliyosajiliwa;

ii) Iwe na kibali cha Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI; na

iii) Isiwe taasisi ya Kimataifa.

### 9.7 Wajibu wa Waangalizi

i) Kutii Sheria, Kanuni na Miongozo ya uchaguzi;

ii) Kutoingilia kwa namna yoyote shughuli za uchaguzi; na

iii) Kuandaa taarifa ya kazi yao na kuiwasilisha Ofisi ya Rais –TAMISEMI ili kupata kibali cha kuisambaza.

**Maswali**

i) Wakala wa chama cha siasa ni nani?

ii) Nini kazi ya Wakala wa chama cha siasa?

iii) Je, ikiwa wakala hatakuwepo katika chumba cha kupigia Kura, kuhesabia Kura na kujumlishia kura zoezi linaweza kuendelea?

## SURA YA KUMI

## MAKOSA NA ADHABU

### 10.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kuelezea makosa mbalimbali ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na adhabu zake.

### 10.2 Makosa ya Uchaguzi

Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa la uchaguzi endapo:

i) Ataharibu orodha ya wapiga kura au nyaraka zozote zinazohusiana na uchaguzi;

ii) Atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji au uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa;

iii) Atajiandikisha zaidi ya mara moja kwenye orodha ya wapiga kura;

iv) Atapiga kura zaidi ya mara moja kwa wagombea wa nafasi moja;

v) Atatishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga uchaguzi;

vi) Atafanya kampeni siku ya uchaguzi;

vii) Ataonesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au Chama cha Siasa katika eneo la mita mia mbili kutoka kwenye kituo cha kupigia kura;

viii) Atamzuia Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Mjumbe wa Kamati ya Rufani au mtumishi wa umma aliyeteuliwa kusimamia uchaguzi kutekeleza majukumu yake;

ix) Atakiuka masharti ya kiapo chake;

x) Atapatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa nafasi moja inayogombewa;

xi) Atavuruga ratiba ya mikutano ya kampeni ya uchaguzi au atavunja masharti ya kampeni za uchaguzi;

xii) Atakutwa na silaha kinyume cha Sheria kwenye eneo la uteuzi wa wagombea, mikutano ya kampeni, eneo la usikilizaji wa rufaa, kituo cha kuandikisha wapiga kura au kituo cha kupigia, kuhesabu na kujumlisha kura;

xiii) Atatangaza matokeo ya uchaguzi kabla hayajatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo kwa mujibu wa Kanuni; au

xiv) Atafanya jambo lolote kinyume cha Kanuni za uchaguzi pamoja na Sheria nyingine za Nchi zinazohusiana na uchaguzi.

**10.3 Adhabu:**

Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote la uchaguzi atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

**10.4 Adhabu kwa kukiuka Taratibu za Maadili ya Uchaguzi**

Kamati za Maadili ya Uchaguzi zinaweza kuchukua hatua zifuatazo:

i) Kuagiza upande uliokiuka maadili kusahihisha kosa au makosa yaliyotendeka na iwapo italazimu, kuomba msamaha hadharani;

ii) Kutoa onyo au karipio kwa maandishi;

iii) Kutangaza jina la Chama au Mgombea aliyekiuka maadili na kueleza kosa au makosa yake kwa njia za Taarifa kwa umma, redio, runinga, magazeti na njia nyingine za mawasiliano; au

iv) Kukisimamisha Chama au Mgombea kuendelea kufanya kampeni za uchaguzi kwa muda itakavyoona inafaa.

**Swali:**

1. Taja makosa ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa.
2. Taja adhabu itakayotolewa kwa atakayekiuka Taratibu za Maadili ya Uchaguzi.